Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu UNM Care na Out-of-County Care

1. Je, UNM Care na Out-of-County-Care ni nini?

UNM Care na Out-of-County-Care ni mipango ya kukusaidia kulipa ada za matibabu kwa huduma za afya katika UNM Hospital. Unaweza kutumia mipango hii ikiwa huna bima na unaweza pia kuitumia hata kama una bima. Mipango hii hulipa ada za matibabu ya dharura na huduma nyingine za afya na matibabu unazoweza kuhitaji. Lengo letu ni kukusaidia kuhakikisha unapata huduma unazohitaji kwa kukusaidia kulipigia gharama.

2. Je, nani anatimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care?

Ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care, unahitaji kuwa mkaaji wa Kaunti ya Bernalillo au Kaunti ya Sandoval.

Ili kutimiza masharti ya kupata Out-of-County Care unahitaji kuwa unaishi katika kaunti nyingine ambayo si Kaunti ya Bernalillo au Kaunti ya Sandoval.

Kwa mipango yote miwili ya UNM Care na Out-of-County Care unahitaji –

- ✓ Kwenda kwenye Hospitali au Kliniki za UNM kwa ajili ya huduma zako za afya na matibabu.
- ✓ Kuwa unapata mapato (ujira, mshahara, malipo ya mipango ya usaidizi) yanayolingana na kiwango fulani au uwe hupati mapato yoyote.

3. Je, ni huduma zipi hulipiwa na UNM Care na Out-of-County Care?

UNM Care na Out-of-County Care hulipia –

- ✓ Huduma za afya, bidhaa na vifaa, matibabu na taratibu zinazohitajika kimatibabu. Gharama zinazohitajika kimatibabu ni pamoja na za bidhaa na vifaa au huduma zinazohitajika ili kutambua au kutibu maradhi yako au kukuwezesha kuendelea kuwa na afya njema. Watoa huduma huamua kinachohitajika kimatibabu.
- ✓ Baadhi ya dawa zinazoagizwa na daktari zinazoweza kuchukuliwa katika maduka ya dawa ya UNM Hospital. Tafadhali muulize mtoa huduma wako iwapo dawa yako inalipiwa na UNM Care au Out-of-County Care.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

4. Je, ni huduma zipi **zisizolipiwa** na UNM Care au Out-of-County Care?

Mipango ya UNM na Out-of-County Care **hailipii** –

- x Dawa zinazoagizwa na daktari zinazochukuliwa katika maduka ya dawa ambayo si ya UNM Hospital
- x Upasuaji wa kuimarisha sura
- x Baadhi ya huduma za kupanga uzazi kama vile –
    - Upasuaji wa kutendua kuhasiwa kwa mwanamume
    - Taratibu za hiari za kuharibu mimba (kuavya mimba)
    - Vipimo na matibabu yanayohusiana na ugumu wa kupata mimba.
- x Huduma za gari la wagonjwa
- x Vifaa vya kimatibabu kama vile vitanda, fimbo au matangi ya oksijeni yanayonunuliwa katika maduka yasiyo ya UNM Hospital. Aina hii ya vifaa inaitwa Vifaa vya Matibabu vya Kudumu (Durable Medical Equipment, DME).

Mkurugenzi wa Matibabu na Afisa Mkuu wa Matibabu wa UNM Hospital wanaweza kuondoa masharti fulani kuhusiana na orodha hii katika hali maalum.

5. Je, nitatumaje ombi la UNM Care au Out-of-County Care?

Hatua ya kwanza ni kujaza ombi. Ili kufanya hivyo, unahitaji kupiga simu kwa **505 272-2521** ili kupanga miadi na Mwakilishi wa Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa. Unaweza kuomba kufanya miadi yako ana kwa ana au kwa simu. Ukikutana na Mwakilishi wako (ana kwa ana au kupitia mawasiliano ya simu), atakusaidia kujaza ombi hilo.

Wakati wa miadi yako, Mwakilishi wako atakusaidia kujaza ombi la UNM Care au Out-of-County Care. Pia atakuambia hati za uthibitisho unazohitaji kuwasilisha pamoja na ombi lako.

Je, nini kitafanyika baada ya hapo?

Tutapitia ombi lako na kuamua ikiwa unatimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care. Ikiwa tunahitaji maelezo zaidi kutoka kwako, tutakujulisha.

Tutakujulisha ana kwa ana au kukutumia barua (taarifa iliyoandikwa) inayokuambia iwapo ombi lako liliidhinishwa. Tutakupigia simu ikiwa ombi lako limekataliwa. **Unapaswa kupokea jibu ndani ya kipindi kisichozidi siku 15 baada ya kupokea ombi lako lililojazwa.**

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Iwapo huna baadhi ya hati, una siku 30 kuanzia tarehe iliyo kwenye fomu inayoitwa “Uthibitisho Unaohitajika (Verification Needed)” (uliyopewa na Mwakilishi wako) ili kuwasilisha hati hizo.

Ikiwa ombi lako litakataliwa kwa sababu hukutimiza masharti, unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu.

6. Je, ninaweza kupanga miadi na kitengo cha Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa ikiwa sina Nambari ya Rekodi ya Matibabu?

Ikiwa tayari una **Nambari ya Rekodi ya Matibabu (MRN)** kwenye UNM Hospital, unaweza kupanga miadi na kitengo cha Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa.

Ikiwa bado huna MRN kwenye UNM Hospital, **ni sawa.** Ambia tu kitengo cha Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa kwamba unahitaji MRN utakapopiga simu kupanga miadi yako ya ombi.

7. Mimi si raia wa Marekani. Je, bado ninaweza kuomba UNM Care au Out-of-County Care kwa ajili ya mtoto wangu au mimi mwenyewe?

Ndiyo! Mtu yeyote anayetimiza sifa zinazohitajika katika mpango anaweza kutuma ombi (tazama Swahili la 2). Hali yako ya uhamiaji **si** sehemu ya mchakato wa kutuma ombi na **si** sehemu ya mchakato wetu wa kufanya uamuzi wa kumwidhinisha au kumkataa mwombaji yeyote.

New Mexico ilipitisha sheria katika mwaka wa 2021 inayosema kwamba watu wote wasio raia (bila kujali hali yao ya uhamiaji) wanaweza kutuma maombi kwa usalama kwa mipango ya usaidizi kama vile UNM Care au Out-of-County Care na hawawezi kunyimwa ufikiaji kwa sababu ya hali yao ya uhamiaji. Unaweza kupata sheria hiyo hapa www.nmlegis.gov/Sessions/21%20Regular/bills/hoU.S.e/HB0112.html.

Ili kulinda faragha yako, **hatutauliza kuhusu hali yako ya uhamiaji**. Hatutaweka taarifa yoyote kuhusu hali yako ya uhamiaji katika ombi lako. Mtu yeyote akikuomba taarifa au hati kuhusu hali yako ya uhamiaji, tafadhali piga simu kwa 505 272-2121.

8. Nikipata usaidizi kutoka kwa UNM Care au Out-of-County Care, je, hilo litaathiri hali yangu ya uhamiaji?

Hapana. Kutumia UNM Care au Out-of-County Care **hakutaathiri** hali yako ya sasa ya uhamiaji au majaribio yoyote katika siku zijazo ya kubadilisha hali yako ya uhamiaji.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Baadhi ya familia huwa na wasiwasi kwamba kupata usaidizi kutoka kwa UNM Care au Out-of-County Care kunaweza kuathiri hali yao ya uhamiaji kwa sababu ya tathmini ya kubainisha iwapo mhamiaji ana uwezekano wa kuhitaji usaidizi wa umma ili kujikimu kimaisha. Kwa sababu UNM Care na Out-of-County Care ni mipango ya usaidizi ya afya, kuitumia kwa ajili yako au mtoto wako hakutaathiri hali yako ya uhamiaji. (Haitachukuliwa kuwa usaidizi unaofaa kuzingatiwa chini ya kanuni ya uwezekano wa mhamiaji kuhitaji usaidizi wa umma ili kujikimu kimaisha.) Unaweza kuomba na ukubali usaidizi kutoka kwa mipango hii kwa njia salama na bila hofu.

9. Je, ninaweza kuomba UNM Care au Out-of-County Care ikiwa mwajiri wangu anatoa bima ya afya?

Ndiyo! Wakati wa kubainisha ustahiki, huwa tunaangalia ukubwa na mapato ya kaya tu. Ikiwa unapata bima kupitia kazi yako, bado unaweza kutuma ombi la UNM Care au Out-of-County Care. Mipango yote miwili inaweza kukusaidia kulipia gharama za kiasi kinacholipwa na mtumiaji wa bima wakati wa huduma na makato kwa huduma za dharura na huduma nyingine za afya na matibabu unazoweza kuhitaji. Si lazima ujisajili kupata bima inayotolewa kazini kwako. Lakini ikiwa ni ya bila malipo, tunapendekeza ujisajili.

10. Ikiwa ninapata msaada wa Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada (Supplemental Nutrition Assistance Program, SNAP), Usaidizi wa Muda kwa Familia Fukara (Temporary Assistance for Needy Families, TANF) na/au Mpango wa Usaidizi wa Lishe kwa Wanawake, Watoto Wachanga na Watoto Wadogo (Women, Infants, and Children, WIC). Je, hilo litaathiri ombi langu la UNM Care au Out-of-County Care?

Ikiwa kwa sasa unapata msaada kutoka kwa SNAP, TANF na/au WIC ya New Mexico, tayari unatimiza sharti la mapato la UNM Care au Out-of-County Care. Kwa hivyo, hutahitajika kutoa uthibitisho wa mapato yako unapotuma ombi. Lakini utahitajika kuthibitisha kwamba unapata SNAP, TANF na/au WIC. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha **yoyote kati ya hati hizi** pamoja na ombi lako –

- ✓ Barua kutoka kwa Idara ya Huduma za Kibinadamu (Human Services Department) kuhusu msaada unaopata
- ✓ Hati ya uthibitisho wa msaada unaopata
- ✓ Picha ya skrini kutoka kwa tovuti ya YES NM ya msaada unaopata

11. Je, ninahitaji kuwasilisha hati zipi ili kuomba UNM Care au Out-of-County Care?

Tunahitaji kuthibitisha wewe ni nani, unakoishi na kiasi cha pesa unachopata. Kwa hivyo, tunakuomba uwasilishe hati fulani za uthibitisho pamoja na ombi lako ili kutusaidia kufanya hivyo.

Wewe ni Nani (Utambulisho)

Tunakuomba uwasilishe hati ya kuthibitisha utambulisho wako. Unaweza kuwasilisha pasipoti yako (kutoka nchi yoyote), leseni ya dereva, kadi ya kitambulisho au aina nyingine ya hati ya utambulisho. Pata maelezo zaidi kuhusu hati tunazoweza kukubali hapa kwa kuangalia kwenye tovuti.

Tafadhali kumbuka –

Tunaomba hati ya uthibitisho wa utambulisho kwa sababu tunahitaji kujua wewe ni nani na kuhakikisha kuwa ni wewe. **Huhitaji** kuwa raia wa Marekani ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care. **Huhitaji** kutuambia hali yako ya uhamiaji na hatutauliza. Hii **haichangii** katika ustahiki wako wa kupata UNM Care au Out-of-County Care.

Ikiwa huna hati inayothibitisha utambulisho wako, ni sawa–tujulishe tu. Tutashirikiana nawe kutafuta suluhisho.

Mahali Unakoishi (Anwani)

Tunakuomba uwasilishe hati iliyo na jina na anwani yako. Kumbuka kwamba unahitajika kuwa unaishi katika Kaunti ya Bernalillo au Kaunti ya Sandoval ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care lakini unaweza kutuma ombi la Out-of-County Care ikiwa unaishi katika kaunti nyingine. Unaweza kuwasilisha waraka ya mshahara, bili ya huduma ya nyumbani, bima ya gari au hati nyingine ambayo ina jina na anwani yako.

Ikiwa huna hati inayothibitisha anwani yako, ni sawa–tujulishe tu. Tutashirikiana nawe kutafuta suluhisho.

Kiasi cha Pesa Unazopata (Mapato)

Tunakuomba uwasilishe hati zinazoonyesha mapato ya jumla ya kila mwezi ya kaya yako. Tunahitaji kujua kiasi unachopata pamoja na kiasi ambacho kila mtu anayeishi nawe hupata. Unaweza kuwasilisha nyaraka za mshahara, fomu za malipo ya kodi, barua au nakala za hundi kutoka kwa mipango ya Social Security, Veterans Affairs, Bureau of Indian Affairs au hati nyingine zinazoonyesha kiasi ambacho kila mtu katika kaya yako hupata, ikiwa ni pamoja na wewe.

Ikiwa huna hati hizi, tafadhali tujulishe tu. Tutashirikiana nawe kutafuta suluhisho.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

Kiasi Ulicho Nacho Katika Akaunti Zako za Benki na za Uwekezaji (Mali)

Tunakuomba uwasilishe hati zinazothibitisha kiasi ulicho nacho katika akaunti zako za benki na za uwekezaji. Ili kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care, huwezi kuwa na zaidi ya jumla ya $20,000 kwenye akaunti zako za benki (za kawaida na za kuweka akiba) na akaunti za uwekezaji kwa pamoja. Unaweza kuwasilisha taarifa za akaunti za hivi karibuni za akaunti zozote za kawaida, za akiba na za uwekezaji ulizo nazo.

Hatutakuomba uchukue pesa kutoka hazina yako ya kustaafu, dhamana, akaunti za kuhifadhi pesa bila kuzichukua kwa kipindi maalum (certificates of deposits, CD) ili kulipia bili zako za matibabu. Hata hivyo, ikiwa tayari umepokea pesa kutoka kwake katika mwaka huo au ikiwa fedha hizo zilifikia kipindi cha kutolewa katika mwaka huo (hii inamaanisha kuwa tarehe imefika ambapo lazima ulipwe kwa uwekezaji wako), fedha hizo zitahesabiwa kama mapato.

Nyumba yako, gari na hazina ya kustaafu havijumuishwi. Huhitaji kuwasilisha hati zozote kuhusu mali hizo.

12. Je, kuna hali maalum ambapo sharti la uthibitisho wa mapato linaweza kuondolewa?

Ndiyo. Ikiwa unapata msaada wa SNAP, TANF au WIC, tayari unatimiza sharti la mapato la UNM Care na huhitaji kuthibitisha mapato yako. Ikiwa huna makazi au umefilisika, tayari unatimiza sharti la mapato na huhitaji kuthibitisha mapato yako.

Lakini huwa tunakuomba utoe maelezo kuhusu hali yako, ikiwa inawezekana. Kwa mfano –

- Ikiwa unapata SNAP, TANF na/au WIC, unaweza kuwasilisha barua kutoka kwa Idara ya Huduma za Kibinadamu (Human Services Department, HSD).
- Ikiwa huna makazi, unaweza kuwasilisha barua kutoka kwa mhudumu wako wa kesi au shirika la jamii linalokujua. Barua ya mfano ambayo mhudumu wako wa kesi anapaswa kutumia inapatikana kwenye tovuti.
- Ikiwa umefilisika, unaweza kuhitajika kuwasilisha hati za mahakama.

Ikiwa huna yoyote kati ya hati hizi, tafadhali tujulishe tu. Tutashirikiana nawe kutafuta suluhisho.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

13. Je, mpango wa UNM Care au Out-of-County Care utalipa bili kutoka kwa hospitali na kliniki ambazo si sehemu ya mfumo wa UNM Hospital?

Hapana. Mipango ya UNM Care na Out-Of-County Care **haitalipia** –

- x Huduma zozote za afya au za matibabu unazoweza kupata **nje ya** UNM Hospital na kliniki zake.
- x Huduma zozote za afya au za matibabu unazoweza kupata katika kliniki hizi ya UNM Medical Group (zilizoorodheshwa hapa chini). Kliniki hizi za Medical Group si sehemu ya UNM Hospital, ingawa baadhi zina UNM katika jina lao.
    - Truman Health Clinic
    - Center for Development and Disability
    - Center for Reproductive Health
    - UNM Center for Life
    - UNM Health Grande Primary Care Clinic
    - DNI Dialysis Clinic

14. Je, ninaweza kupata usaidizi kutoka kwa UNM Care au Out-of-County Care kwa muda gani?

Unaweza kupata usaidizi kutoka kwa **UNM Care** kwa **mwaka 1**. Kipindi hicho cha mwaka 1 huanzia tarehe tutakayoidhinisha ombi lako. Mwishoni na mwaka 1, unaweza kutuma ombi upya. Mchakato wa kutuma ombi upya ni wa haraka na rahisi zaidi.

Kwa **Out-of-County Care** unaweza kupata usaidizi kwa **miezi 6**. Kipindi hicho cha miezi 6 huanzia tarehe tutakayoidhinisha ombi lako. Mwishoni na miezi 6, unaweza kutuma ombi upya.

15. Je, itakuwaje ikiwa nina bili kutoka kabla ya nilipoidhinishwa?

Ukipata huduma za tiba (miadi, utaratibu, matibabu) ndani ya **kipindi cha miezi 6 kabla ya** kuidhinishwa kupata UNM Care au Out-of-County Care, tunaweza kukusaidia kulipia gharama ya huduma hizo mradi huduma hizo –

- ✓ Zilikuwa zinahitajika kimatibabu (huduma za dharura na huduma nyingine za afya na za matibabu unazoweza kuhitaji).
- ✓ Zilipokewa katika UNM Hospital au kliniki zake.

This translation was completed by LanguageLine Solutions.

Swahili

16. Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji huduma za matibabu huku nikisubiri kupata habari kuhusu iwapo ninatimiza masharti?

Unaweza kwenda katika UNM Hospital na kliniki zake kwa huduma za matibabu huku ukisubiri kujua ikiwa unatimiza masharti na tutalipa bili baada ya kuidhinishwa kwako. Lakini ukikosa kuidhinishwa, utawajibika kulipa bili hizo. (Tazama Swali la 18 kwa taarifa kuhusu mapunguzo ya gharama na mipango ya malipo.)

Au unaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Ombi lako likikataliwa, tutakutumia barua inayoeleza sababu. Ukiamua kukata rufaa, tutapitia ombi lako upya. Unaweza kupata hati ya ombi la kukata rufaa kwenye tovuti.

17. Je, ninaweza kupata hati na taarifa za usaidizi wa kifedha za UNM Care na Out-of-County Care katika lugha nyingine?

Ndiyo! Ikiwa unataka hati zozote kati ya hizi kwa lugha nyingine, tafadhali tembelea tovuti. Nyingi **zimetafsiriwa** na unaweza kuzipata.

Ikiwa unazungumza lugha nyingine na unataka **mkalimani**, tafadhali tujulishe! Tuna wakalimani wa ana kwa ana wa Lugha ya Ishara ya Marekani, Kihispania, Kinavajo na Kivietinamu. Tunaweza pia kukuunganisha na wakalimani wanaotoa huduma kwa simu na video wa takriban lugha yoyote ile. Huduma za mkalimani zinatolewa bila malipo. Ni haki yako kisheria kupata mkalimani wa lugha unayopendelea.

18. Je, ombi langu la UNM Care au Out-of-County Care ni la siri?

Ndiyo! Ombi lako na maelezo yote unayotoa katika mchakato wa ombi ni ya siri. UNM Hospital haitayashiriki. Maelezo hayo yatatumiwa na UNM Hospital tu na **hayatapeanwa** kwa wahusika wengine wowote nje ya UNM Hospital.

19. Je, itakuwaje nikikosa kutimiza masharti ya kustahiki lakini nisiwe na pesa za kutosha kulipia bili zangu za matibabu?

Ikiwa unaishi New Mexico na ukose kutimiza masharti ya kupata UNM Care au Out-of-County Care na huna bima, utapata kiotomatiki **punguzo la malipo ya kujilipia mwenyewe**.

Punguzo la malipo ya kujilipia mwenyewe hupunguza ada za hospitali na daktari kwa asilimia 45 (45%). Kwa hivyo, kwa punguzo hilo, bili yako itakuwa kiasi kidogo tu juu ya nusu ya gharama ya kwanza.

Pia tunaweza kukusaidia kubuni **mpango wa malipo** unaokuruhusu kulipa bili zako za matibabu polepole muda unavyosonga badala ya kulipa kiasi chote mara moja. Tutakusaidia kupata mpango unaokufaa wewe na bajeti yako na hatutakutoza riba. Piga simu kwa 505 272-2521 kwa taarifa zaidi kuhusu mipango ya malipo.

20. Je, nitapataje taarifa zaidi au kupata usaidizi wa kushughulikia mchakato wa kutuma ombi?

Ikiwa unataka taarifa zaidi, unahitaji usaidizi au una maswali kuhusu yoyote kati ya taarifa hizi, unaweza kufanya yafuatayo:

Nenda kwenye tovuti yetu

Nenda kwenye https://unmhealth.org/patients-visitors/billing-insurance/ kwa taarifa zaidi kuhusu UNM Care na Out-Of-County Care. Pia utapata taarifa kuhusu kutuma ombi la UNM Care, Sera ya Usaidizi wa Kifedha, hati nyingine muhimu na tafsiri za hati hizi huko.

Tupigie simu

Piga simu kwa **505 272-2521** au **877 909-6661** (bila malipo) Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa mbili asubuhi (8:00 am) hadi saa kumi na moja jioni (5:00 pm). Ikiwa unahitaji mkalimani, tujulishe tu. Huduma za ukalimani zinapatikana kwa lugha nyingi.

Tutembelee

UNM Hospital Patient Financial Services
1131 University Blvd NE, Suite D
Albuquerque, NM 87102